# LEARNING BY EAR

# "WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA"

## KIPINDI CHA NANE: "VITA DHIDI YA MGENI MSOALIKWA"

**SCRIPT: CHRISPIN MWAKIDEU**

**EDITOR: ANDREA SCHMIDT**

**ASSISTANT EDITOR: KATRIN OGUNSADE**

**HEALTH EXPERT: DR.HEIDRUN HÜBNER**

**List of characters for episode 8:**

- MASIKA (40),
- BETTINA (34),
- KAREMBO (14),
- ZAWADI (BABY, no actor)
- DAVID (14),
- MAMA DAVID (43)
- YAKUBU (41)
- H/TEACHER (38, female)
- DR. MUNGA (45, male)

**INTRO/NARRATOR:**

Kwa mara nyingine tena nakuamkia msikilizajui popote pale unaposikiliza kipindi chetu cha **Noa Bongo jenga maisha yako. Tukiwa bado katika mchezo wa kuigiza** " WAGENI V**IZABIZABINA MSOALIKWA- IKIWA NI VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA".** Kipindi kilichopita, tuliiacha familia ya Masika ikiwa imesharudi nyumbani na binti yao Karembo baada ya kuuguwa kwa muda hospitali kutokana na malaria kali. Bado uhasama na jirani yao mamake david unatokota na usisahau ndiye aliyekuwa mshauri mkuu wa mkewe masika na kumshawishi aende kwa mganga wa kienyeji mizanja. Kwengineko nako masika anashindwa kuwashauri upya wavuvi wenzake kukoma kuzitumia neti za kujikingia mbu katika shughuli zao za uvuvi. Na aliposikiliza redio kuhusu malaria, Masika alikuwa na swali kwa dkt munga.. Tega sikio uifuatilie familia ya masika ikielekea nyumbani ili tujuwe yatakayojiri.... " **katika kisa ''VITA DHIDI YA WAGENI WASOALIKWA"**

**MUSIC INTERLUDE**

**<u>SCENE ONE: MASIKA'S FAMILY IN PUBLIC TRANSPORT GOING HOME</u>**

**A-SFX: TRAFFIC NOISE/HOOTING AND MOTOR ENGINES REVVING, DRIVING NOISE FROM INSIDE THE CAR**

1. **BETTINA/KAREMBO: (BOTH LAUGHING)**

2. **BETTINA:** Masika..Mume wangu. **(GIGGLES)** ulikuwa unafikiria nini kuuliza swali kama lile? Na ulikuwa makini mno **(IMITATES MASIKA'S VOICE)** bwana dkt..eeh.. samaki wanaweza kutumiwa kuwadhibiti mbu?

3. **MASIKA:** Unasema nilifikiri nini? Nilikufikiria wewe na wanangu,sitaki kuwaona mukiteseka tena.. na hujui daktari Munga alinieleza nini ulipoondoka na karembo, lakini nilipata elimu mpya na sikuwa jura kama unavyodhania.

4. **KAREMBO:** Kwa hivyo ulijifunza nini baba? Tueleze na sisi pia.

5. **MASIKA:** Dkt. alinieleza kuwa samaki wanaweza kutumiwa kuangamiza mbu... kwa kuyala mayai yao yanayotagwa majini... kwa hivyo nataka niweke samaki mbuta katika kila kidimbwi kilichoachwa bila matumizi ambamo mbu wanataga mayai yao huko... unajuwaje, siajabu pia nikapata soko kubwa kwa kuwauza samaki hao watakapozaana na siatahitaji tena kwenda baharini kuvua samaki

6. **KAREMBO:** Shabash! Hilo ni wazo zuri! Kazi yangu itakuwa kuwalisha kila asubuhi.

7. **MASIKA:** Hapatokuwa na haja yakuwalisha kwani watakuwa wakila hayo mayai ya mbu... mpaka tutakapokuwa na hakika kuwa wameyamaliza mayai yote ya mbu ndio uanze kuwalisha .... unaonaje betina? Hebu nikusaidie kumbeba zawadi, unaonekana mchovu...

8. **B-SFX: BABY STARTS TO CRY IN LOW SLEEPY VOICE**

**9. MASIKA:** Nitambeba tutakaposhuka garini.
(**TO CONDUCTOR)**
tafadhali manamba tushushe kituo kinachofuata na tuna mizigo juu ya gari.

**NARRATOR:** Basi familia ya Masika ilishuka na kujitipa mizigo yao vichwani na kuelekea nyumbani.. lakini walipofika..

**10. C-SFX: FUMBLING OF KEYS, DOOR BEING OPENED**

**11. KAREMBO:** Nyumbani ni nyumbani..wacheni nikapumzike kidogo kitandani.

**12. BETTINA:** **(NOTICES SCREEN ON WINDOW)**
Hmm mumewangu... naona umenunuwa neti ya kuzuia mbu madirishani? Hebu kidogo! Ela hili sio rinda langu la harusi?
**(ANGRILY)**
Masika, mbona unanifanyia hivi? Unalitundika vipi rinda langu la harusi dirishani?

**13. MASIKA:** Wacha hamaki,mke wangu.nilikuwa najaribu kuona kama litazuia mbu kuingia..na imewezekana!tangu nilitundike rinda lako la harusi mbu wameadimika kama maziwa ya kuku,hata hivyo sidhani kama una mpango wakulivaa tena ama?

**14. BETTINA:** **(SCREAMING)**

Haijalishi! Wewe una ubinafsi! Kwanza uliichukuwa neti ya kukingia mbu ukaenda kuivulia samaki, sasa umelichukuwa rinda langu la harusi eti wazuia nalo hao hao mbu.. na yote haya uliyafanya nikiwa siko hapa nyumbani….

**15. MASIKA:** Mke wangu... rinda ni kitu unachoweza kununua tena lakini uhai haununuliki... nitairudisha neti nyumbani na kuitia upya dawa ya kuua wadudu... na kama ni hili rinda tulitumie kwa sasa mpaka tutakapopata pesa za kununua neti ya dirishani. mrarukiwa ndiye fundi wa kukunja mkewangu..

**NARRATOR:** Baada ya mzozano huo, siku mbili zilipita na karembo akawa amepata afueni kamili baada ya kumaliza dozi alizotakiwa kutumia na akarudi shule. Alikuwa akiwaeleza wenzake yaliojiri na ghafla kengele ikalia bali kutarajiwa,wanafunzi wote wakajipanga milolongo kama ilivyo desturi kusikiliza mwito huo.

<u>**SCENE TWO: SCHOOL ASSEMBLY PITCH**</u>

**16. D-SFX: EMERGENCY BELL RINGS FOLLOWED BY NOISE FROM STUDENTS**

**17. H/TEACHER:** **(ALOUD)**

Kimya!,kila mmoja anyamaze!

(**PIN DROP SILENCE)**

Nyote munafahamu kuwa eneo leo ndilo lililokumbwa mno na gonjwa hili la malaria... siku chache zilizopita, nilikwenda kumtembelea mmoja wa wanafunzi wetu bora Karembo katika hosipitali

ya tarafa ambaye alikuwa amelazwa kwa ajili ya malaria.. nafurahi kuwaeleza kuwa amepata nafuu na amerudi shuleni... leo kabla ya kuanza utaratibu wetu wa masomo.. nimemuelika mtu muhimu sana. Atajielza kwetu yeye ni nani na atueleze amekuja kutuletea ujumbe gani....

**18. E-SFX: CLAPPING FOLLOWED BY APPLAUSE WITH WHISTLES ETC.**

**19. DR. MUNGA:** Asanteni... majina yangu ni Dkt.Munga.. ninafanya kazi katika hospitali ya tarafa ya Ribo na sitotaka kuwapotezea muda wenu mwingi... mwalimu wenu mkuu alinialika nije niwape ushauri wa kitaalamu kuhusu ugonjwa wa malaria,ningependa tufanye mahojiano... sasa, ni nani anaweza kunieleza ni njia gani mtu anaweza kuambukizwa malaria? Ukiwa unalojibu tafadhali nyoosha mkono.

**20. DAVID:** Tunapata malaria kutokana na mbu.

**21. DR. MUNGA:** Sawa, lakini hujatupa jibu kikamilifu... ni mbu gani haswa wanaoambukiza malaria..

**22. KAREMBO:** **(THINKING)**
Ni mbu wa kike anayeitwa Anoflesi anayehitaji damu ili kutaga na kukuza mayai yake..

**23. DR. MUNGA:** Sawa Sawa!

**NARRATOR:** Hatua kwa hatua Dkt Munga aliwazungumzia wanafunzi hao kuhusu malaria,akijadili ninani miongoni mwetu aliyeko hatarini zaidi kuambukizwa Malaria na kwanini..aliwaeleza jinsi ya kujikinga kwa njia zote zinazotumika. pia alizungumzia kuhusu dawa za kutibu maambukizi na dalili za malaria ni zipi... hatimaye, aliwatakia kila la heri katika masomo na mitihani yao na kuwahimiza kuwa bidii yao masomoni ni muhimu kwani wao ndio madaktari, wahandisi, mawakili na marubani wa kesho.. Kando na hapo.. masika alikuwa na harakati zake za kuweka samaki mbuta katika vidimbwi vya kufugia samaki vilivyokuwa havitumiki.

**24. F-SFX: OCCASIONAL SPLASHES FROM FISH**

| | | |
|---|---|---|
| **25.** | **YAKUBU:** | Ewe!<br>**(CALLS OUT)**<br>Masika!mbona wataka kutushangaza.unafanya nini sasa? |
| **26.** | **MASIKA:** | **(SARCASTICALLY)**<br>Nacheza karata!,kwani wewe waona nafanya nini? |
| **27.** | **YAKUBU:** | Mbona wajifanya jura? Wajuwa vyema kuwa hao samaki watakufa wote kwa sababu huna fedha za kuwanunulia chakula...utawalisha nini!? |
| **28.** | **MASIKA:** | Ndio, ni kweli kuwa sina fedha.. lakini sihitaji pesa kuwalisha... humu mwenye vidimbwi muna chakula tosha! |

**29. YAKUBU:** (**SURPRISED)**
kweli? Sasa chakula hicho kiwapi? Mimi naona vijidudu na mbu tu...

**30. MASIKA:** Kumbe wajua tena hao mbu hutaga mayai humu majini... hayo mayai ndio chakula cha hawa samaki.. **(PROUDLY)** na pindi samaki watakapokuwa wakubwa nitawachukuwa na kuwauza... lakini hilo sio lengo kuu la kufanya hivi... pindi mayai yatakapoliwa.. basi idadi ya mbu bila shaka itapunguwa...

**31. YAKUBU:** (**LAUGHS OUT)**
kwa hivyo umekuwa mtu wa mazingira? Sikiliza, malaria si maradhi mapya hapa petu.. tumekuwa nayo tangu..aah hata sijui... hakuna yeyote atakayeizuia . kwaheri... mimi naelekea baharini...

**NARRATOR:** Mabadiliko hayachukuliwi kwa urahisi mahali popote.. lakini japo mwenye lake haachi... akiacha halioti... ndivyo wavyele walivyojinaki... lakini kama Masika amepata kisomo ..basi haitachukuwa muda wengine kujiunga naye... baada ya shule siku hiyo, karembo na david walirudi nyumbani pamoja.

**<u>SCENE THREE: KAREMBO AND DAVID GOING HOME.</u>**

**32. G-SFX: STORM BUILDING FOLLOWED BY RAINFALL**

**33. DAVID:** Karembo, Tafadhali njoo ujikinge mvua na mwavuli wangu... usije ukanyeshewa ukapata

homa... nilifurahi sana kukuona shuleni.. sote tulifurahi. tulikuwa na wasiwasi...

34. **KAREMBO:** Asante David,wajua nini?nini wazo,na nahitaji msaada wako.

35. **DAVID:** Chochote usemacho... unajua mimi tangu kitambo..

36. **KAREMBO:** **(CUTS HER SHORT)**
Hapo hapo! Tafadhali niahidi kuwa hautanizungumzia tena hayo maneno... sisi sote ni wadogo... tutakapaojihusisha na mambo ya mapenzi hivi sasa tutaathiri masomo yetu.. sikiliza, wazo langu ni kuhusu kuanzisha chama cha kupambana na malaria shuleni kwetu... ulimsikia dkt munga, alisema kuwa vita dhidi ya malaria vinahitaji kila mmoja wetu... kwa hivyo tutaanza chama na tujifunze kuhusu malaria, alafu tutapanga ziara na kuielimisha jamii kuhusu kukata vichaka, tuyaondoshe maji yaliyokita, au chochote kitakachotusadia kupambana na malaria... unasemaje?

37. **DAVID:** **(HESITANT)**
Aaah... sijui karembo... unajuwa mamangu ni....

38. **KAREMBO:** Najuwa, lakini kwanza zungumza na yeye, Alafu nijulishe... ni muhimu tukiwa pamoja na wewe katika chama .

**39. DAVID:** (**EXCITED**

Mwanachama pamoja na wewe?!,Nikifika nyumbani tu.. nitamueleza mamangu!

**40. KAREMBO:** Nitaanza kazi punde tu nitakapofika nyumbani... nitakata nyasi ndefu karibu na nyumba yetu... na maji yote yaliyotuwa nitayaondowa...nimetangaza vita dhidi ya wageni vizabizabina wasoalikwa!.

**41. DAVID:** **(IMPRESSED)**
Inaonekana umejitolea muhanga... labda ukiendeleza juhudi zako unaweza kuja kupata tuzo la Nobeli kwa mchango wako.. **(GIGGLES)**

**42. KAREMBO:** Nituzwe au nisipotuzwa,najua sote tunaweza kuchangia vita hivi dhidi ya malaria.na mimi naanza hivi sasa!,Asante kwa mwavuli.tuonane kesho,shuleni.

**43. H-SFX: RAIN LESSENS.**

**MUSIC INTERLUDE**

**OUTRO/NARRATOR:**

Mpaka hapo ndio tunafika mwisho wa sememu ya nane ya mchezo ” **”WAENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA”.** Lakini vitimbi bado vinaendelea... je, mamake david atasemaje baada ya kuelezwa mtazamo wa karembo na mwanawe David? Je,karembo atapata wafuasi katika chama hicho cha kupambana na malaria? Kwengineko,je masika atafua dafu katika mradi wake huo wa kuangamiza mayai ya mbu? Usikose kujiunga nasi tena katika sememu ya tisa ya mchezo huo na usisahau ukipenda

kusikiliza tena au kutupa maoni yako kuhusu uliyoyasikia tembelea tovuti yetu anuani ni www.dw-world.de/lbe.
Hadi wakati mwengine..kwaheri.